
# UCHAGUZI

Jarida la Tume ya Taifa ya Uchaguzi Toleo Na. 02 Aprili, 2022



## Baraza la Wafanyakazi

Tume kuongeza ufanisi na uwajibikaji ili tija iweze kuonekana katika utekelezaji wa shughuli.

IFAHAMU TUME

# KUASISIWA KWA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

Mwaka 1991 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ali Hassan Mwinyi aliteua Tume ya kwanza chini ya Uenyekiti wa Marehemu Jaji Mkuu Mstaafu Francis Nyalali. Madhumuni ya Tume hii ilikuwa kukusanya maoni ya wananchi juu ya kuendelea na mfumo wa chama kimoja au kuwa na mfumo wa vyama vingi.

Kutokana na ushauri wa Tume ya Nyalali, Sura ya 3 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ilirekebishwa na kufanya Tanzania kuwa Taifa linalofuata mfumo wa Vyama vingi vya Siasa.

Sheria ya Vyama vya siasa, (Na. 5 ya mwaka 1992) ilirekebishwa ili kuwezesha kuandikishwa kwa vyama vya siasa. Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, (Na.1 ya mwaka 1985), Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa,(Na. 4 ya mwaka 1979) na sheria zinazoendana pia zilirekebishwa ili kuondokana na matakwa ya chama kimoja na kuruhusu mchakato wa kufanyika kwa Uchaguzi chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Tarehe 13 Januari 1993, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilianzishwa chini ya Ibara ya 74(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Wajumbe wa Tume waliteuliwa kwa mara ya kwanza tarehe 14 Januari 1993

 Toleo la Aprili, 2022

# Baraza la Wafanyakazi

***Na Mwandishi wetu***

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Dkt. John Jingu amewataka watumishi wa Tume kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika sehemu zao za kazi ili tija iweze kuonekana katika utekelezaji wa shughuli zao.

Akifungua kikao cha baraza la wafanyakazi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kilichofanyika Machi 31, 2022 jijini Dodoma, Katibu Mkuu amewakumbusha watumishi wa Tume agizo alilolitoa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan wakati akipokea ripoti ya TAKUKURU na ile ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Serikali ya kuzingatia weledi, uwajibikaji na tija katika sehemu zao za kazi.

Dkt. Jingu amesema kila mtumishi wa umma amepewa nafasi ya kutekeleza majukumu yake kulingana na vipaji na sifa za weledi wake katika kazi. Hivyo, amewataka watumishi hao kutimiza majukumu yao ipasavyo.

“Endapo watendaji mtaamua kutekeleza majukumu yenu kwa kuzingatia weledi na uwajibikaji ni dhahiri kuwa tija itaonekana kazini,” alisema Dkt.Jingu.

Akizungumzia umuhimu wa kikao hicho, Dkt. Jingu aliwataka



wajumbe wa baraza la wafanyakazi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutambua kuwa baraza hilo ni kiungo muhimu katika kukuza ustawi na maendeleo ya Tume, hivyo wahakikishe kuwa wanawawakilisha vyema wenzao ambao hawapo kwenye kikao hicho kwani wana mategemeo makubwa kutoka kwao.

Aidha, Katibu Mkuu aliwapongeza viongozi na watumishi wote wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuchapa kazi kwa ufanisi mkubwa, na pia alimpongeza kwa namna ya kipekee Mwenyekiti Mstaafu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Mhe. Jaji Rufaa (Mst) Semistocles Kaijage kwa utumishi wake na Mhe Jaji wa Mahakama ya Rufani Jacobs Mwambegele kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambaye pia ni Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume, Dkt. Wilson Mahera Charles aliwataka wajumbe wa baraza hilo kutambua dhamana waliyopewa ya kuwa kiungo kati ya uongozi na watumishi wa Tume na kutekeleza jukumu hilo ipasavyo.



Aliongeza kuwa Tume itahakikisha kuwa watumishi wake wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi, weledi na uwajibikaji na kwamba uongozi utahakikisha kuwa maslahi ya watumishi wa Tume yanazingatiwa.

# Siku ya Wanawake

***Na Mwandishi wetu***

Tarehe 8 Machi, 2022 wafanyakazi wanawake wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi waliungana na wenzao kusherehekea siku yao adhimu ambayo imekuwa ikitumika kufanya mambo mbalimbali ya kuwakutanisha wanawake kote duniani kujadili mambo mbalimbali yanayohusu ustawi wao.

Kama sehemu ya maadhimisho hayo, siku ya tarehe 07 Machi, 2022 wanawake wa Tume walitembelea kituo cha kulelea watoto yatima cha Kijiji cha Matumaini kilichopo eneo la Kisasa jijini Dodoma.

Wakiwa kituoni hapo wanawake hao walizungumza na uongozi wa kituo, watoto na baadae wakakabidhi zawadi mbalimbali.

Mwanzilishi wa kituo hicho, Padri Vicent Boseil aliwashukuru wanawake hao kwa msaada walioutoa na kutenga muda wao kuwatembelea watoto hao.

Katika kilele cha maadhimisho hayo, Wanawake hao walijumuika na wenzao kusherehekea siku hiyo ambayo kimkoa ilifanyika Wilayani Chemba, mkoa wa Dodoma ikiwa na kaulimbiu ya "Kizazi cha Haki na Usawa kwa Maendeleo Endelevu; Tujitokeze kuhesabiwa".

Akizungumza wakati wa maadhimisho hayo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Bw. Anthony Mtaka alisema Serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni moja kwa Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya kufanikisha zoezi la anuani za makazi, ikiwa ni maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi.

Bw. Mtaka alisema serikali imefanya hivyo ili kuhakikisha tukio hilo linafanyika kama ilivyokusudiwa na kuleta matokeo chanya, akahimiza wananchi wote bila ubaguzi kujitokeza kwa wingi katika maeneo yao kuhesabiwa.



*Wawakilishi wa wanawake kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakiwa kwenye picha ya pamoja na watoto yatima wanaolelewa kwenye Kijiji cha Matumaini kilichopo Kisasa jijini Dodoma.*



Toleo la Aprili, 2022

# Maadili kwa Watumishi



*Afisa kutoka Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi Makao Makuu, Fabian S.Pokela (Aliyesimama) akifafanua jambo mbele ya watumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati wa mafunzo ya siku moja ya maadili kwa watumishi wa Tume yaliyofanyika jijini Dodoma Tarehe 23 Machi,2022.*

***Na Mwandishi wetu***

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Dkt. Wilson Mahera Charles amewaasa watumishi wa umma kuzingatia sheria, taratibu na maadili ya utumishi wa umma pale wanapokuwa wanatekeleza majukumu yao.

Akizungumza na watumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi hivi karibuni wakati wa mafunzo ya siku moja ya watumishi hao kuhusu uadilifu wa watumishi wa serikali, Dkt. Wilson Mahera Charles amesema kuwa mafunzo hayo ni muhimu kwa watumishi hao kwani Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni taasisi inayotekeleza majukumu

yake kwa kuzingatia maadili.
Amesema mafunzo hayo yanawakumbusha watumishi wa umma kuzingatia maadili katika utekelezaji wa majukumu yao na hivyo kuboresha shughuli za utoaji huduma kwa wadau mbalimbali wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.
Naye, mtoa mada katika mafunzo hayo Bw. Fabian Pokela amesema kuwa Serikali imedhamiria kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma katika taasisi mbalimbali nchini ili kuwakumbusha watumishi wa umma kuhusu dhamana waliyopewa katika kuwatumikia watanzania huku wakifuata misingi bora ya utumishi.
Alisema watumishi wa umma wanapaswa kufanya tathmini juu ya huduma wanazozitoa kwa wananchi ili kuboresha pindi mapungufu mbalimbali yanapojitokeza.
Pokela aliwaasa watumishi wa umma kuhakikisha kuwa wanatambua mambo yanayoathiri ubora wa huduma katika utendaji wa taasisi zao hususan kupatikana au kutopatikana kwa huduma husika, kujali muda na kuzingatia viwango vya huduma inayotolewa.
Kwa upande wake Mkurugenzi wa Utawala na Raslimali Watu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Bw. Gerald Mwanilwa aliwashukuru watoa mada kwa kutoa mafunzo kwa watumishi kwani yatawaongezea uelewa wa sheria, taratibu na maadili ya utumishi wa umma.
Mbali na mada ya uadilifu kwa watumishi wa umma, mada inayohusu mgongano wa maslahi kwa watumishi wa umma iliwasilishwa na kujadiliwa kwa kina.



# Ushirikiano na Asasi

*Na Mwandishi wetu*

Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) limeishukuru Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kufungua milango kwa wadau wa uchaguzi kutoa maoni yao na kujifunza mambo mbalimbali yanayohusiana na utendaji wa Tume.



Shukrani hizo zimetolewa hivi karibuni na Mratibu wa Kitaifa wa WiLDAF, Bi. Anna Kulaya alipoongoza ujumbe wake kwenye mkutano na sekretarieti ya Tume kujadili mambo mbalimbali ikiwemo uelewa wa sheria za uchaguzi.

Bi. Kulaya alisema ni mara ya pili taasisi yake imepata fursa ya kukutana na sekretarieti ya Tume na katika vikao hivyo amejifunza kwamba Tume inaendeshwa kwa uwazi na kwamba uongozi wa Tume upo tayari kila wakati kusikiliza na kutoa ufafanuzi kwa wadau wake.

"Tunawashukuru sana kwa kutukaribisha tena kwa mara nyingine, majadiliano yetu yamekuwa mazuri na yenye tija. Tumejifunza mambo mengi hasa kuhusiana na sheria za uchaguzi,"alisema.

Mchechemuzi wa WiLDAF, Bw. Deus Kibamba kwa upande wake alisema kwamba kupitia mazungumzo hayo wamejifunza kwamba Tume inaendeshwa kwa uwazi na inatoa ushirikiano mzuri kwa wadau wake.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Kisheria wa Tume, Bw. Emannuel Kawishe aliuhakikishia ujumbe huo kwamba Tume itaendelea kuweka milango yake wazi kwa wadau mbalimbali wanaohitaji kujifunza juu ya utendaji wake.

# Utafiti wa REPOA

***Na Mwandishi wetu***

Taasisi ya REPOA imetoa matokeo ya utafiti kuhusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ambapo imeipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kufanya yanayohusiana na uandikishaji wa wapiga kura, utoaji wa elimu ya Mpiga Kura, uendeshaji wa Uchaguzi Mkuu na kujitokeza kwa Wapiga Kura siku ya Uchaguzi.



vizuri kwenye kuratibu, kuendesha na kusimamia uchaguzi huo.

Utafiti huo ulijikita kwenye mambo

Kwenye utafiti huo ambao matokeo yake yamewasilishwa Tume hivi karibuni, REPOA imebaini

kuwa asilimia 63 ya wapiga kura walikuwa wamepata ujumbe wa Elimu ya Mpiga kura kuhusu Uchaguzi Mkuu siku chache kabla ya siku ya kupiga kura.

Utafiti umeainisha kwamba asilimia 50 ya ujumbe huo ulitolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na asilimia 7 ulitolewa na Asasi za Kiraia na asilimia 41 ulitolewa na watu wengine.

Aidha, utafiti huo umeonesha kuwa asilimia 36 ya Wapiga kura walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, ambapo asilimia 58 hawakuwa na uelewa wa kutosha na asilimia 7 ya wapiga kura hawakuwa na maoni yoyote kuhusu Uchaguzi huo.

Utafiti pia umeonesha kwamba kati ya asilimia 80 ya Wapiga Kura waliohojiwa kuhusiana na kuridhika na utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura, asilimia 52 walijibu kuwa wametosheka sana na utoaji huo wa Elimu na asilimia 27 walijibu wameridhika kiasi jambo ambalo linaashiria kwamba Tume imefanya vizuri katika utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura.

Kuhusu Wapiga Kura walioandikishwa, asilimia 65 walikuwa na uelewa juu ya uwekaji wazi wa Daftari la Awali la wapiga kura ambapo kati ya hao, asilimia 91 ya wapiga Kura walikagua taarifa zao za Mpiga Kura na asilimia 82 kati ya waliokuwa na taarifa ya kuwekwa wazi kwa Daftari la Awali la Wapiga Kura walikuwa wanahitaji taarifa zaidi za Uboreshaji wa Daftari.

Pia, kuhusu kujiamini kwa Wapiga kura katika mchakato wa uandikishaji wa Wapiga Kura, asilimia 92 walikuwa wakijiamini kwa kiwango cha juu na asilimia 78 ya hao wapiga kura walijiamini kuwa taarifa zao zimeingizwa kwenye Daftari kwa usahihi na aslimia 10 taarifa zao zilikosewa.

Aidha, kwenye eneo la upigaji kura, utafiti unaonesha kwamba asilimia 78 ya wapiga kura walijitokeza kupiga Kura ambapo asilimia 54 ni kutoka maeneo ya vijijini na asilimia 24 ni kutoka mijini na kati ya hao waliopiga kura, asilimia 41 ni wanaume na asilimia 38 ni wanawake.

REPOA wameipongeza Tume kwa kutoa Elimu ya Mpiga Kura mpaka maeneo ya Vijijini tofauti na watu wengine wanavyodhani kuwa Elimu ya Mpiga Kura inatolewa zaidi mijini kwa sababu ndiko kwenye vyombo vingi vya habari na miundombinu mizuri ya kuwafikia Wapiga Kura.

Kuhusu ulinzi na usalama katika mchakato mzima wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, asilimia 84 ya Wapiga Kura waliohojiwa walieleza kuwa usalama ulikuwa umeimarishwa sana na asilimia 6 walieleza kuwa Ulinzi na Usalama haukuimarishwa vya kutosha.

# MICHEZO

## NEC yajipima Nguvu



*Mchezaji wa timu ya NEC FC, Desmond Haukila (katikati) akijaribu kuwahadaa walinzi wa Timu ya Chuo Kikuu cha Dodoma wakati wa mchezo wa kirafiki ulizozikutanisha timu hizo mbili hivi karibuni katika uwanja wa Informatics uliopo Chuo Kikuu cha Dodoma.*

***Na Mwandishi wetu***

Timu za mpira wa miguu na pete za Tume zimecheza michezo ya kujipima nguvu hivi karibuni na kuzidi kujiimarisha.

Timu ya Mpira wa Miguu ilicheza michezo miwili dhidi Timu ya watumishi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH FC) na kutoka sare ya bila kufungana na pia ilicheza na timu ya Watumishi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM FC) na kutoka sare ya 2-2.

Kwa upande wa timu ya mpira wa pete, timu hiyo ilifungwa 50-6 na



*Mchezaji wa timu ya Mpira wa Pete wa NEC Queens, Dainess Nkenjah akijaribu kudaka mpira wakati wa mchezo wa kirafiki na Timu ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM Queens) uliochezwa hivi karibuni katika uwanja wa Informatics uliopo Chuo Kikuu cha Dodoma.*

kutoa changamoto kwa timu hiyo kujipanga na kujiandaa vyema na Michuano ya MEI MOSI inayotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Michezo mingine waliyocheza ni dhidi ya watoza kodi wa TRA ambapo NEC FC ilikubali kichapo cha bao 6-3 huku dada zao NEC Queens wakiibuka kidedea kwa kuwacharaza TRA Queens bao 18-14.

Mwenyekiti wa Klabu ya Michezo ya Tume, Bw. Juvenile Kaiza amesema matokeo ya Michezo hiyo yamewafanya waongeze zaidi bidii mazoezini ili kuondoa mapungufu ambayo walimu waliyaona kwa timu zote mbili.

Aidha, Bw. Kaiza amesema timu ya mchezo wa kuvuta kamba nayo imeanza mazoezi ya kujiandaa na michuano ya MEI MOSI.

"Tumeendelea kujifua kimichezo, hii ikiwa ni pamoja na timu ya kuvuta kamba na riadha ili kujiweka sawa kwa ajili ya michezo ya MEI MOSI ambayo ipo mbele yetu, ambayo tunataraji kushiriki", alisema Kaiza.

Kaiza pia amewahimiza watumishi na wanamichezo wote kujitokeza katika mazoezi kwani kufanya hivyo kutawaweka vizuri kimchezo na pia kuimarisha afya zao.




Tume ya Taifa ya Uchaguzi
Makao Makuu Dodoma,
5 Barabara ya Uchaguzi,
41107 Njedengwa,
Uchaguzi House,
Anuani: S.L.P 358, Dodoma
Namba ya simu: +255 26 2962345-8
Nukushi: +255 26 2962348
Barua pepe: Uchaguzi@nec.go.tz

www.nec.go.tz tumeyauchaguzi_tanzania

Tume ya Uchaguzi-TZ Tume ya Uchaguzi-tz NEC online TV